

HALMASHAURI YA WILAYA USHETU

SHULE YA SEKONDARI DAKAMA

S.L.P. 20

USHETU – KAHAMA

Barua pepe:dakamasecondaryschool@gmail.com

- SIMU NA. 1. MKUU WA SHULE 0766 759224 / 0620539153
2. MAKAMU MKUU WA SHULE: 075787848 / 0765 643460
3. MATRON: 0764 615416 / 0688299300
4. PATRON: 0764 922310 / 0620 183041

Kumb. Na. DSS/ADM/FVS/VOL.VI/2022/2023

JINA LA MWANAFUNZI: _____

S.L.P. _____

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DAKAMA KIDATO CHA
TANO (5) MWAKA 2022/2023**

Kwaniaba ya watumishi wote wa shule ya sekondari Dakama, ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha tano (5) mwaka 2022/2023. Aidha natumia fursa hii kukupongeza na kukukaribisha sana kwenye shule yetu. Shule hii ni ya Serikali na ni ya mchanganyiko (Co – Education). Shule ina wanafunzi wa bweni kwa kidato cha tano na sita ikiwa na tahasusi za PCM, PCB, HGL,HGK na HKL na ina wanafunzi wa kutwa wa kidato cha kwanza hadi cha nne.

Shule ya sekondari Dakama iko Km 23 kusini mwa mji wa Kahama kandokando ya barabara iendayo Ulowa au Kashishi – Urambo kutokea Kahama Mjini, na Km 3 kabla ya kufika senta ya Iboja yalipo Makao Makuu ya Kata ya Ukune na Tarafa ya Dakama .

Shule hii ipo pembeni mwa mji, mahali patulivu na pazuri sana kwa kusoma na kujifunza. Unatakiwa kusoma kwa bidii sana kutimiza lengo la Taifa. Mheshimiwa BENJAMINI .W. MKAPA Raisi wa awamu ya 3 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema – nanukuu “ **Tunafanya kila tuwezalo kuwapeni elimu, lakini uamuzi wa kutumia elimu hiyo ni wenu. Tambueni kuwa upo mzigo mkubwa wa kuendesha nchi hii unawasubiri. Jiandaeni vizuri, someni kwa makini msituangushe na zaidi sana msipate ukimwi. Thamani yenu ni kubwa sana na ni ya kudumu. Msiipoteze kwa tamaa za mwili zipitazo.**”

USAFIRI

Usafiri kutoka Kahama Mjini kuja shuleni ni wa uhakika kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni kwa mabasi makubwa na madogo yapitayo shuleni Dakama kuelekea Iboja. Utashushwa shuleni kabisa (**DAKAMA SEKONDARI**). Nauli halali ni TShs 3,000/= kwa mabasi makubwa na Tsh.4,000 kwa mabasi madogo, Magari haya hupatikana kwenye kituo cha mabasi ya abiria kilichopo eneo litwalo DODOMA maarufu kama stendi ya DODOMA. Magari yote yaendayo Ulowa, Makazi, Kashishi kupitia IBOJA yatakufikisha shuleni. Usipande magari yaendayo Bulungwa, Butibu au Idahina. Hakikisha unapanda magari yanayopitia **Iboja** kisha omba ushushwe shuleni Dakama kabla ya kufika Iboja. Usafiri wa pikipiki, bajaji upo japo ni ghali.

MUHULA WA KWANZA

Muhula wa masomo utanza Septemba 2022. Unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe iliyobainishwa na Wizara. Wanafunzi wa kidato cha tano watakochelewa zaidi ya muda uliobainishwa na Wizara hawatapokelewa. Wizara itajaza nafasi hizo kwa kuwapa wanafunzi wengine.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. SARE YA SHULE (DARASANI)

A. WASICHANA

- Njoo na sketi mbili (2) ndefu za dark blue (grade one) zinazokaribia kisigino / kifundo cha mguu (MAMA SAMIA STYLE), mshono wa linda boksi, sketi fupi hazikubaliki. (**Rejea kiambatanisho A**) mwishoni mwa fomu hii
- Mashati mawili (2) meupe ya mikopo mifupi / nusu kanzu nyeupe kwa atakayetumia hijabu.
- Soksi nyeupe jozi mbili (2) fupi za kati
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika na kufunga kwa gidamu (kamba)
- Rangi ya hijabu na kikofia chake iwe nyeupe kwa atakaye tumia na izingatie maadili ya kidini (Ndefu) kwa ajili ya darasani.
- Sweta rangi ya dark blue.
- Hijabu nyeusi na kofia yake nyeusi kwa ajili ya kushindia kwa atakayetumia na izingatie maadili ya kidini (ndefu).

B. WAVULANA

- Njoo na suruali mbili (2) rangi ya dark blue, suruali iwe na malinda mawili kila upande mbele, pia iwe imekunjwa chini (turn up) na yenye upana usiopungua inchi 16”, suruali za chupa hazikubaliki (**Rejea kiambatanisho A**).

NB: Suruali isiyofikia upana wa inchi 16” haitapokelewa

- Soksi nyeupe jozi mbili (2) fupi za kati
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika na siyo buti wala ghorofa (High Heeled Shoes) vya kufunga kwa gidamu (Kamba)
- Mashati meupe (2) mikono mifupi
- Sweta rangi ya dark blue

2. A: ADA YA SHULE

- Tshs 70,000/= kwa mwaka na TShs 35,000/= kwa muhula
- Ada ilipwe kwenye Benki ya NMB au wakala wa NMB A/C 30601200112
JINA LA AKAUNTI – DAKAMA SECONDARY SCHOOL CAPITATION

B: MICHANGO YA SHULE

- Tahadhari Tshs 5,000/= hii hairudishwi,hufidia uchakavu anwai mwanafunzi awapo shuleni.
- Kitambulisho TShs 5,000/=
- Taaluma Tshs 10,000/= kwa mwaka
- Ulinzi Tshs 5,000/= kwa mwaka
- Matibabu Tshs 30,000/= kwa mwaka (haijalishi una bima ya afya au hauna)
- Maji Tshs 28,000/= kwa mwaka
- Umeme Tshs 20,000/= kwa mwaka
- Ukarabati TShs 15,000/= kwa mwaka

MICHANGO ILIPWE BENKI YA NMB: A/C NA. 30601100137

JINA LA AKAUNTI YA MICHANGO: DAKAMA SECONDARY SCHOOL FUND

NB; Njoo na risiti mbili (2) za benki, moja ya ada na nyingine ya michango yote

3. VITABU:

Mwanafunzi wa kidato cha tano PCM ,PCB , HGL ,HGK na HKL anashauriwa kuja na vitabu muhimu kwa tahasusi yake kwa matumizi binasfi. **(Rejea kiambatanisho C)**

4. VITU VINGINE MUHIMU VYA KUJA NAVYO

- (i) Rimu mbili (2) za karatasi nyeupe (A4) kwa mwaka
- (ii) Form four (IV) Result Slip (Original)
- (iii) Pesa za matumizi binasfi
- (iv) Scientific Calculator kwa tahasusi za PCM,PCB,HGK na HGL
- (v) Rula na mathematical Set kwa tahasusi zote
- (vi) Mfagio mmoja wa chelewa (mgumu) wenye mshikio wa mti kwa wanafunzi wote.
- (vii) Lekio moja kwa wanafunzi wa PCM na PCB
- (viii) Ndoo moja ya lita 20 kwa kila mwanafunzi
- (ix) Jembe moja (01) na mpini mmoja (01) kwa wanafunzi wa HGL na HGK
- (x) Squeezer moja (01) kwa wanafunzi wa HKL

MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI

NA	MAHITAJI
1	Godoro la sponji futi $2\frac{1}{2}$ X 6
2	Blanketi kwa ajili ya baridi
3	Sanduku la chuma
4	Ndoo moja kwa ajili ya usafi binafsi
5	Mashuka manne (4), mashuka mawili ya rangi ya pinki na mawili ya light blue
6	Taulo, chupi au boxer za kutosha
7	Sabuni za kutosha
8	Mafuta ya kupaka
9	lesso
10	Ndala / sendo / open shoes
11	Kiwi na brashi
12	Mswaki na dawa ya meno
13	Kitana
14	Kikombe cha uji / chai cha nusu lita
15	Kijiko
16	Sahani na bakuli
17	Chandarua cha mstatiri na siyo duara (ring) rangi ya ligh blue kwa wavulana na wasichana rangi ya pinki
18	Daftari kubwa (Counter Books quire 4) sita na kalamu za kutosha
19	Sketi mbili (2) za kushindia rangi ya kijivu (Grade one) zinazovuka magoti, mshono wa linda boksi kwa wasichana (Rejea kiambatanisho A)
20	Suruali mbili (2) za kushindia rangi ya kijivu (Grade one) zenye marinda mawili mbele kila upande, iwe na turn up na yenye upana usiopungua inchi 16”, suruali chupa hazikubaliki (Rejea kiambatanisho A)
21	Tochi / kurunzi (Isiwe ya kuchaji kwa umeme).
22	Track suit pea moja (rangi ya bluu bahari)
23	Kitenge doti moja (wasichana)
24	Soksi jozi mbili rangi nyekundu kwa ajili ya michezo. Vifaa na mavazi ya michezo kama raba na Jezi rangi ya light bluu. Ni lazima kila mwanafunzi aacheze isipokuwa kwa ushauri wa Daktari
25	T-shirt za shule (darasani & kushindia) zinapatikana kwenye duka la shule

Tanbihi

1. Mwanafunzi aje na Bank Pay in Slip mbili (Ada na michango) ambazo zina jina la mwekaji ambalo ni jina la mwanafunzi husika
2. Mwanafunzi asije na nguo za nyumbani na simu haziruhusiwi kabisa
3. Mahitaji ya vitu vidogo vidogo yapatikana au yanauzwa kwenye duka la shule
4. Fika mapema shuleni (kaba ya saa 12:00 jioni) ili uweze kupokelewa na kupewa huduma mara ufikapo
5. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa track suit anaporipoti shuleni na si vinginevyo

6. Mwanafunzi ahakikishe amepima afya yake na kujaziwa fomu iliyoambatanishwa na maelezo haya kwenye hospitali au kituo cha afya cha serikali na siyo binafsi
7. Kila mwanafunzi nilazima awe na **Bima ya Afya NHIF au CHF na bima zingine zinazotambulika**
8. **Wanafunzi wakike wanaruhusiwa kusuka nywele za kurudi nyuma (kuanzia mistari minne (04) na isizidi mistari sita (06), kusuka siyo lazima.**

MWL COSMAS .J. CHAMOTO

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi au utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- (c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Night Preparation)
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- (i) Kutunza mali za Umma

MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
- (e) Kupigana au kupiga
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa
- (h) Kuwa mjamzito / kupata mimba
- (i) Kuoja au kuolewa
- (j) Kutoa mimba
- (k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
- (l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (m) Kutumia au kumiliki simu ya mkononi


. , \$0 %\$7\$1 , 6+2 \$ 6\$5(

: \$98/ \$1\$: \$6, &+ \$1\$



: \$98/ \$1\$

: \$6, &+ \$1\$



KIAMBATANISHO B
OR – TAMISEMI
USHETU DISTRICT COUNCIL
DAKAMA SECONDARY SCHOOL
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

To the Medical Officer

Date _____

From _____

Name of student in full _____ please examine the above as to his / her physical and mental fitness for a full time study (two years course)

The examination should include:-

- (i) (a) Eye – sight (b)Hearing (c) Speech (d) Limbs (e)Chest (f) Veneral Diseases (g) Epilepsy (h) Leprosy
- (ii) Cirrhosis
- (iii) Other diseases
- (iv) Pregnancy (For ladies)

PART B (To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named person and consider that he / she is physically and mentally **FIT / UNFIT** for a full time of four years study / course.

- (i) (a) Eye – sight _____
(b) Hearing _____
(c) Speech _____
(d) Chest _____
(e)Veneral Diseases _____
(f) Epilepsy _____
(g) Neurosis _____
- (ii) (a) Neurosis _____
(b) Cirrhosis _____
- (iii) Other serious diseases _____
- (iv) Pregnancy _____

PART C

Doctor's General Remarks _____

Signature: _____ Designation _____ Station _____

KIAMBATANISHO C

ORODHA YA VITABU KWA KILA SOMO

1. HISTORIA

- ✓ Saleh Yassin (2010), Essentials in Advanced Level History One & History Two
- ✓ Zisti Kamili (2010) History Advanced Level History One & History Two
- ✓ Shibitali C.K (2012) Contemporary historical Events, Advanced Level History Two & History One

2. JIOGRAFIA

- ✓ Monk House (1990) The principle of Physical geography
- ✓ David Waugh (2009) practical Geography
- ✓ David Waugh (2009) Integrated Approach Physical Geography
- ✓ Zist Kamili (2010) Physical Geography Alive for Advanced level
- ✓ Zist Kamili (2010) Human and Economic Geography
- ✓ Mtegetwa (20010) Practical Geography
- ✓ Msabila D.T (2020 Practical Geography for Advanced Level
- ✓ Msabila D.T. (2010) Human and Economic Geography
- ✓ Pritchard John (2000) Practical Geography for East Africa
- ✓ Pritchard John (2000) Economic Geography for East Africa

3. ENGLISH LANGUAGE

- ✓ Advanced Level Literature (Nyambari Nyangwine (2012)
- ✓ Nicholous Asheli, Practical Approach, Literature (2012)
- ✓ Betrayal in the City , Francis Imbuga
- ✓ Selected Poems – TIE
- ✓ An enemy of the people – Henrik Ibsen
- ✓ A hand out for Advance, Paschal Salaw, need Level English One
- ✓ I will Marry when I want – Ngugi wa Thiong’o
- ✓ A man of the People – Chinua Achebe
- ✓ The Beautiful Ones Are Not Yet Born – A. Armah
- ✓ A season by Waiting – David Omowale
- ✓ Advanced Level Literature – Nicholous Asheli
- ✓ The Wonderful Surgeon and Other Poems by Charles Mloka
- ✓

4. BAIOLOJIA

- ✓ Taylor, D.J et al (2009) Biological science one & two 3rd Ed, Cambridge university Press, Edinburgh
- ✓ Toole, G and Toole, S (1999) Understanding Biology for advances, level
- ✓ Plants and animals biology vol I & II
- ✓ Chand, S, Verna P.S and Pandey (2010) Biology for class IX
- ✓ Botany for degree students by Dutta

- ✓ Clegg, C.J and Mackean, D.G (1994): Advanced Biology, Principles and applications John Murray publishers LTD

5. KEMIA

- ✓ TIE (2019, Organic chemistry for A-level Secondary Schools
- ✓ TIE (2019), Inorganic Chemistry for A-Level Secondary Schools form five & six
- ✓ TIE (2019), Physical Chemistry for A – Level Secondary Schools form five & six
- ✓ TIE (2019) General Chemistry for A-Level Secondary School form five & six
- ✓ Ramsden, E.N (2000). Advanced level chemistry (3rd ed). Cheltenham: Nelson Thrones publishers Ltd

6. FIZIKIA

- ✓ Chand for class Xi and Xii
- ✓ Tom Duncan
- ✓ Rodger Muncaster
- ✓ Nelcon
- ✓ Recipicious Kiiza

7. ADVANCED MATHEMATICS

- ✓ Sillen S.I (2014) Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools – FV, FVI (GDY Publications Company Ltd DSM
- ✓ Tranter C.J (2006) “ Advanced Level Mathematics 4th edition, Hroder Murray, London NW 1 3BH
- ✓ Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools by Tellem Majigwa

8. GENERAL STUDIES

- ✓ J,K (1974) Ujamaa – Essays on socialism, London Oxford University Press
- ✓ Saluhaya M.C (2003) Advanced Level General Studies
- ✓ Nyambari N (2018) Advanced Level GS notes form 5 and 6 Nyambari Nyangwine Publishers DSM
- ✓ Mkapa B.W (2019), My life, My purpose: Mkuki na Nyota Publishers, DSM

9 . KISWAHILI

1. Nadharia ya lugha ya Kiswahili: Kidato cha Tano na Sita – Nyambari Nyangwine na Masebo (2010)
2. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuho – Kihore, Y.M. na Masamba, D.P.B: TUKI (2003)
3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili: English – Swahili Dictionary – TUKI
4. Sarufi miundo ya Kiswahili (SAMIKISA) – Masamba, D.P.B.
5. Nadharia ya Fasihi kidato cha Tano na Sita – Masebo - +Oxford University Press
6. Tahakiki Vitabu Teule Vya Fasihi Kidato cha 5 na 6 – Nyambari Nyangwine na Masebo

TAMTHILIA (WALAU VITABU VIWILI)

1. Kivuli kinaishi – Said Ahmed Mohamed – Oxford University Press
2. Kwenye Ukingo wa Thimu – Ibrahim Hussein – Oxford University Press
3. Nguzo Mama – Penina Muhando (1982)
4. Morani – Emanuel Mbogo (1993)

RIWAYA (WALAU VITABU VIWILI)

1. Vuta ni kuvut, 4th ed. – Mbunda Msokile (2009)
2. Kufikirika, 4th ed. – Shaban Robert – Mkuki na Nyota
3. Mfadhili – Hussein Tuwa (2007) – Macmillan Aidan
4. Usiku utakapokwisha, 2nd ed. – Mbunda Msokile (2007) – Macmillan Aidan

USHAIRI (WALAU VITABU VIWILI)

1. Kimbunga: Toleo la Tatu (3rd ed. – Haji Gora Haji (1995) – TUKI
2. Chungu Tamu – Theobald Mvungi
3. Mapenzi Bora – Shaban Robert – Mkuki na Nyota publishers
4. Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu – Macmillan Aidan